

**JAMHURI YA MUUNGANO WA TANZANIA**

**BUNGE LA TANZANIA**



**ORODHA YA SHUGHULI ZA LEO**

**MKUTANO WA TATU**

**KIKAO CHA HAMSINI NA TANO**

**21 JUNI, 2021**



## ORODHA YA SHUGHULI ZA LEO

### MKUTANO WA TATU

KIKAO CHA HAMSINI NA TANO – TAREHE 21 JUNI, 2021

I. DUA:

II. MASWALI:

OFISI YA WAZIRI MKUU:

455. MHESHIMIWA MICHAEL COSTANTINO  
MWAKAMO (KIBAHA VIJIJINI):

Atamuuliza Mheshimiwa Waziri Mkuu:-

Je, Serikali ina mkakati gani wa kuwasaidia Watumishi waliostaafu kupata mafao yao kwa wakati.

OFISI YA RAIS (TAMISEMI):

456. MHESHIMIWA ANASTAZIA JAMES  
WAMBURA (VITI MAALUM):

Atamuuliza Mheshimiwa Waziri wa Nchi, Ofisi ya Rais (TAMISEMI):-

Je, ni lini ujenzi wa Shule za Sekondari utaanza katika Kata zisizo na Shule za Sekondari nchini ili kuendana na mpango wa Serikali wa kuhakikisha kila Kata inakuwa na Shule ya Sekondari.

**457. MHESHIMIWA NOAH LEMBURIS SAPUTU (ARUMERU MAGHARIBI):**

Atamuuliza Mheshimiwa Waziri wa Nchi, Ofisi ya Rais (TAMISEMI):-

Je, ni lini Serikali itatekeleza ahadi ya Mheshimiwa Rais ya ujenzi wa Barabara ya Redio Habari Maalum kwenda Hospitali ya Wilaya ya Olturumet kwa kiwango cha lami.

**WIZARA YA MAJI:**

**458. MHESHIMIWA STELLA SIMON FIYAO (VITI MAALUM):**

Atamuuliza Mheshimiwa Waziri wa Maji:-

Je, Serikali ina mpango gani wa kupeleka Mradi mkubwa wa maji katika Mji wa Tunduma ili kutatua changamoto wanayoipata Wakazi wa Mji huo.

**WIZARA YA AFYA, MAENDELEO YA JAMII,  
JINSIA, WAZEE NA WATOTO:**

**459. MHESHIMIWA STELLA IKUPA ALEX  
(VITI MAALUM):**

Atamuuliza Mheshimiwa Waziri wa Afya,  
Maendeleo ya Jamii, Jinsia, Wazee na  
Watoto:-

Je, ni lini Serikali itaandaa utaratibu mzuri wa  
Matibabu kwa Watu Wenye Ulemavu wakati  
ikisubiri Bima ya Afya kwa wote.

**WIZARA YA UJENZI NA UCHUKUZI:**

**460. MHESHIMIWA FLATEI GREGORY MASSAY  
(MBULU VIJIJINI):**

Atamuuliza Mheshimiwa Waziri wa Ujenzi na  
Uchukuzi:-

Je, ni lini Serikali itaanza ujenzi wa Barabara  
ya Mbulu - Hydrom – Singida kwa kiwango cha  
lami ambayo ni ahadi ya Mheshimiwa Rais  
tangu Mwaka 2015.

**461. MHESHIMIWA DKT. PIUS STEPHEN  
CHAYA (MANYONI MASHARIKI):**

Atamuuliza Mheshimiwa Waziri wa Ujenzi na  
Uchukuzi:-



Je, Serikali ina mpango gani wa kuanza ujenzi wa Barabara ya kutoka Manyoni – Sanza – Chipanga – Bahi hadi Dodoma kwa kiwango cha lami.

**462. MHESHIMIWA STANLAUS HAROON NYONGO (MASWA MASHARIKI):**

Atamuuliza Mheshimiwa Waziri wa Ujenzi na Uchukuzi:-

Je, ni lini Serikali itaanza ujenzi wa Barabara ya *Bypass* ya Mji wa Maswa.

**WIZARA YA MIFUGO NA UVUVI:**

**463. MHESHIMIWA ANGELINA ADAM MALEMBEKA (VITI MAALUM):**

Atamuuliza Mheshimiwa Waziri wa Mifugo na Uvuvi:-

- (a) Je, ni asilimia ngapi ya mapato yatokanayo na Uvuvi wa Bahari Kuu yanaenda upande wa Zanzibar;
- (b) Je, kwa miaka 5 iliyopita Zanzibar imepata kiasi gani.

## **WIZARA YA MALIASILI NA UTALII:**

### **464. MHESHIMIWA JOSEPH GEORGE KAKUNDA (SIKONGE):**

Atamuuliza Mheshimiwa Waziri wa Maliasili na Utalii:-

Je, ni lini Serikali itazalisha Mbegu za Mti wa Mninga ili Wananchi waweze kupanda na kuzalisha Miti hiyo kibiashara.

### **III. HOJA ZA SERIKALI:**

#### **WAZIRI WA FEDHA NA MIPANGO:**

Kwamba, Bunge sasa likubali Kujadili Hali ya Uchumi wa Taifa kwa Mwaka 2020 na Mpango wa Maendeleo wa Taifa kwa Mwaka wa Fedha 2021/2022.

Kwamba, Bunge sasa likubali Kupokea na Kupitisha Makadirio ya Mapato na Matumizi ya Serikali kwa Mwaka wa Fedha 2021/2022.

***(Majadiliano yanaendelea)***

**DODOMA  
21 JUNI, 2021**

**N.J. MWIHAMBI, *ndc*  
KATIBU WA BUNGE**